

FOMU YA MAOMBI YA KUVUNA MITI KIBIASHARA

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA (TFS)**

Picha ya
mwombaji

Anwani ya Simu: "TFS",
Simu Na: +255 22 2864249
Fax: Na. +255 22 2864255
Barua pepe mpingo@tfs.go.tz



FOMU YA MAOMBI YA KUVUNA MITI KIBIASHARA

**(Fomu ya maombi imendaliwa kwa kuzingatia Kanuni Namba 3 ya Kanuni za Misitu, 2004;
Tangazo la Serikali Na. 69 la tarehe 9/06/2006; Tangazo la Serikali Na. 59 la tarehe
28/01/2022 na Tangazo la Serikali Na. 173 la tarehe 04/05/2018)**

A: MASHARTI KWA MWOMBAJI

**(Masharti yamewekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Misitu, 2004 na Tangazo la
Serikali Na. 69 la tarehe 9/06/2006)**

1. Awe na mashine iliyoruhusiwa kisheria kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 53 ya Kanuni za Misitu 2004 pamoja na marekebisho yaliyopo katika Tangazo la Serikali Na. 69/2006.
2. Mwombaji kabla hajasimika mashine anapaswa kuzingatia kanuni ya 53(9) na (10) ikisomwa pamoja na jedwali la 33 ya Kanuni za Misitu 2004.
3. Maombi yote yatumwe kwa anuani husika ya Mhifadhi Mkuu wa Shamba (Kiambatisho Na. 1)
4. Mgao ambao hautavunwa kwa kipindi cha miezi minne (4) utahamishwa kwa mteja mwingine
5. Fomu ya maombi itakayotumwa Makao Makuu ya Wizara ya Maliasili na Utalii au Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) haitashughulikiwa.
6. Picha ya mwombaji itakayoambatishwa na fomu hii lazima ithibitishwe na Afisa Mtendaji wa kijiji/Mwenyekiti wa Mtaa/Wakili/ Afisa kabidhi wasii na viapo.
7. **Ada ya maombi ya fomu itakayolipwa haitarudishwa.**

B: MAELEZO BINAFSI /KAMPUNI/KIKUNDI

- a) Jina la mwombaji /Kampuni/ Kikundi
- b) Anwani ya mwombaji S.L.P Wilaya Mkoa
- c) Nambari ya simu Barua pepe
- d) Tarehe ya kuzaliwa
- e) Kama ni kampuni taja tarehe ya kusajiliwa na namba ya usajili
- f) Uraia
- g) Nambari ya passpoti (Kama siyo raia wa Tanzania)
- h) Mahali ilipotolewa Muda wa kuisha
- i) Je, una leseni ya biashara ya mazao ya misitu kutoka wilaya husika? Ndiyo/Hapana (Futa isiyotakiwa)

C: MAELEZO YA VITENDEA KAZI

- a) Je, una mashine ya kuchakata magogo/miti?. Ndiyo/Hapana (Futa isiyohusika)
- b) Taja eneo na ambatisha kibali cha kusimikwa mashine kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania
- c) Taja aina ya mashine na uwezo wake wa kupasua ujazo wa magogo kwa mwaka
- d) Weka alama ya vema kama mashine unayomiliki ina sehemu zifuatazo:
Loading bench ()
Breakdown saw ()
Receiving bench ()
- e) Je, una magari ya kubebwa magogo? Ndiyo /Hapana. (Futa isiyotakiwa). Kama unayo magari ambatisha kivuli cha kadi ya gari au mkataba wa kukodi gari.

D: MAELEZO YA WATAALAMU WA KIWANDA NA MAHALI UNAPOOMBA KWENDA KUVUNA

- a) Je, una mtaalamu wa misumeno? Ndiyo / Hapana (Futa isiyotakiwa).
- b) Je, una fundi mwendesha mitambo (trained operator)? Ndiyo / Hapana.
- c) Kama ndiyo, taja chuo alichopata ujuzi huo na ambatisha kivuli cha cheti cha mafunzo aliyohitimu
- d) Je, una fundi wa mitambo (Technician)? Ndiyo/Hapana.

E: MAELEZO YA MAHITAJI YA MALIGHAFI UNAYOOMBA

- a) Miti migumu (Misaji, Mikaratusi, Loliondo “Olea”)
Weka kiwango cha ujazo unaoomba
Meta za ujazo

- b) Miti laini (Misindano)
Weka kiwango cha ujazo unaoomba
Meta za ujazo

F: VIAMBATISHO NA MUDA WA KUREJESHA FOMU

- a) Mwombaji binafsi anayeendelea kuvuna ambatishe uthibitisho wa mlipa kodi (Tax clearance)
- b) Endapo ni Kampuni, ambatanisha nakala ya hati ya ukaguzi wa hesabu (Certified Audited Financial statement)
- c) Fomu ya maombi irejeshwe kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba husika kabla ama ifikapo tarehe **27 Juni, 2023** saa tisa na nusu (09:30) mchana.

G: GHARAMA YA MAOMBI YA FOMU YA KUVUNA MITI KIBIASHARA

Mwombaji alipie fomu hii kulingana na ukubwa wa kiwanda (Jedwali Na. 1). Malipo yote yatafanyika kwenye akaunti za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) zilizopo kwenye benki ya **NMB, NBC, CRDB na Benki ya Posta** kupitia Mfumo wa **GePG (Government electronic Payment Gateway)** baada ya kupewa Hati ya Madai kutoka shamba husika. Kadhalika, Hati ya Madai imeonesha **mitandao ya simu** inayoweza kutumika kulipia maduhuli ya serikali. Risiti ya malipo iambatishwe na fomu wakati wa kuituma kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba husika.

Jedwali Na. 1: Ada za maombi ya uvunaji (Application fees)

MAHITAJI NA AINA YA KIWANDA	KIWANGO CHA ADA (TSHS)
Viwanda vikubwa vyenye Mikataba na Serikali	200,000.00
Viwanda zaidi ya meta za ujazo 5,000 –	150,000.00
Viwanda kuanzia meta za ujazo 3,001 hadi 5,000	140,000.00
Viwanda kuanzia meta za ujazo 1,001 hadi 3,000	120,000.00
Viwanda kuanzia meta za ujazo 1 hadi 1,000	100,000.00

NB. Unapofanya malipo ya maombi haya zingatia Kipengele E ya ujazo ulioomba uende sambamba na malipo yatakatofanywa.

Imetiwa saini na:

Jina **Saini** **Tarehe**